



# JOHN MERLANI SECONDARY SCHOOL

MISSIONARIES OF THE PRECIOUS BLOOD

P.O. Box 2010

DODOMA – TANZANIA

Registration N° S 4880, NECTA Exams N° S 5391

tel. 0766 939 536

e-mail: [jmerlinisec@gmail.com](mailto:jmerlinisec@gmail.com)

web-site: [cppseducation.sc.tz](http://cppseducation.sc.tz)

## FOMU YA OMBI LA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

Shule ya sekondari John Merlani ipo Miyuji, Jijini Dodoma. Inamilikiwa na Shirika la Wamisionari wa Damu Azizi. **Ni shule ya mseto** (Wasichana na Wavulana), **ni ya Bweni**. Ni shule inayofanya vizuri sana Kitaaluma na malezi ya watoto. Kitaaluma ipo kwenye tano bora za Mkoa wa Dodoma kwa vidato vyote. Na hakuna mhitimu aliyetokea kufeli katika shule hii.

Passport

Fomu hii inapatikana shuleni John Merlani, Parokia ya Kisasa, Nkuhungu na Redio Mwangaza hapa Dodoma. Kwa Dar es salaam inapatikana Parokia za Tegeta, Boko, Bahari Beach, Kunduchi Mtongani na St. Gaspar Mbezi Beach. Gharama ya Fomu ni **Tshs. 15,000/=** ya kulipwa kwa njia ya Benki.

- JINA LA BENKI: **NMB**
- JINA LA ACCOUNT: **JOHN MERLANI SECONDARY SCHOOL**
- NAMBA YA ACCOUNT: **52010026469**

Siku ya mtihani wa kijiunga na shule uje na pay in slip ya Benki.

Mtihani wa Kujiunga na shule (entrance tests) utafanyika shuleni John Merlani (Dodoma), Parokia ya Kunduchi Mtongani Dar es salaam na Saint Gaspar college Morogoro Jumatatu ya tarehe 12/10/2020 kuanzia saa 1:30 asubuhi. Wanoachaguliwa kujiunga na shule mwaka 2021 ni wale tu waliofaulu kwa alama isiyo chini ya **30** katika **kila somo (Hesabu, Sayansi, English)**. Ili kujiunga na shule yetu mwaka 2021, kusoma Pre-Form One ni lazima. Pre-Form One itaanza tarehe 02/11/2020 hadi 18/12/2020. Wote pia wanapaswa kukaa Bweni. Gharama ya Pre-form One kwa muda huo ni Tshs. 300,000/= Malipo ni kwa njia ya Benki.

Ada ya shule kwa mwaka 2021 ni Tshs. 2,000,000/= (milioni mbili). Michango inayochangishwa na serikali haipo ndani ya ada. Ada inaweza kulipwa kwa awamu moja (Januari siku shule ikianza) au awamu mbili (Januari na Julai) au kwa awamu tatu (January, Aprili na Julai). Ada yote iishe kulipwa mwezi Julai. Malipo yote ni kwa njia ya Benki.

Urudishe fomu hii kabla ya siku ya mtihani wa kujiunga shuleni au siku ya mtihani wenyewe.

### **MAELEKEZO:**

Jina la Mwanafunzi.....

Jina la Baba Mzazi au Mlezi .....

Jina la Mama Mzazi .....

Tarehe – mwezi – Mwaka wa kuzaliwa .....

Mwaka wa kumaliza elimu ya Msingi .....

Namba ya Mtihani wa Darasa la VII .....

Shule ulipomaliza elimu ya msingi .....

Namba ya simu ya mzazi au Mlezi .....